2

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA

MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA TAREHE 29.6.2017

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1	Mhe	Charles M. Nyambita	-	M/Kiti H/Wilaya ya Musoma
2	Mhe	Flora R. Yongolo	-	Mkurugenzi Mtendaji (W)-Katibu
3	Mhe	DeboraZ. Mogaya	-	Mjumbe
4	Mhe	Neema C. Jandwa	-	Mjumbe
5	Mhe	Ekwabi D. Michael	-	Mjumbe
6	Mhe	Rajabu M. Mchele	-	Mjumbe
7	Mhe	Paul S. Charamba	-	Mjumbe

WAJUMBE WASIOHUDHURIA

1	Mhe	Wegoro Musiba	-	Makamu/M/Kiti H/W – Kwa taarifa
2	Mhe	Mambo J. Rebule	-	Mjumbe – kwa taarifa
3	Mhe	Prof. Sospeter Muhongo	-	Mbunge – kwa taarifa

WATAALAM WALIOHUDHURIA

1	Ndg	Sophia Manyaki	-	Afisa Uchaguzi (W)
2	Ndg	Paul B. Makuri	-	Afisa Kilimo (W)
3	Ndg	Remin Tarimo	-	Mhandisi ujenzi (W)
4	Ndg	Sarah Sablack	-	Kaimu Afisa Mifugo (W)
5	Ndg	M.E. Nyaindi	-	Usafi na Mazingira
6	Ndg	Buzana Kazare	-	Afisa Ugavi
7	Ndg	Jesse Mwangwa	-	Kaimu mweka Hazina (W)
8	Ndg	George ogutu	-	Afisa Elimu Sekondari (W)
9	Ndg	Thadeus makwanda	-	Kaimu Mganga Mkuu (W)
10	Ndg	Joachim Stewart	-	Kny: Afisa Utamaduni
11	Ndg	Emanuel masanja	-	Mhandisi maji (W)
12	Ndg	Paschal Jagadi	-	Mkaguzi wa ndani (W)
13	Ndg	Pendo Tongora	-	Kny: Afisa Elimu Msingi (W)
14	Ndg	Tibezuka F. Katalyeba	-	Kny: Afisa Mipango (W)
15	Ndg	John Kindia	-	Afisa Maliasili (W)
16	Ndg	Abdulatif Rajabu	-	Kaimu Afisa/M/jamii (W)
17	Ndg	Mary Alexander	-	Afisa Utumishi (W)
18	Ndg	Andrew mbasa	-	TEHAMA
19	Ndg	Aggrey manga	-	Afisa Tawala
20	Ndg	Hamis Manyerere	-	Mwandishi wa Mikutano

KUMB.NA. KFUM/08/2016/2017/113 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 6.32 mchana na kuwafahamisha wajumbe kwamba kikao hiki kimechelewa kuanza kutokana na majukumu mbalimbali ya kiserikali, hata hivyo aliwataka wajumbe kuwa wasikivu ili kumaliza kikao mapema.

KUMB.NA. KFUM/08/2016/2017/114 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA.

Muhtasari wa kikao cha kawaida cha tarehe 29.5.2017 uliwasilishwa na kupokelewa, uliwekewa saini kama kumbukumbu sahihi.

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/115 YATOKANAYO

1. **KUSAFISHWA KWA STENDI MPYA YA BUKIMA, BUSEKERA MUGANGO NA PIA MINADA.**

   Ilifahamika kwamba mhandisi wa ujenzi (W) alikutana na mkandarasi wanaolima barabara na kuwaomba kusaidia kusafisha maeneo ya stendi katika maeneo ya Busekera, Mugango na Bukima, hata hivyo wakandarasi hao wamekubali kwamba wakiwezeshwa mafuta watafanya kazi hiyo. Kwa upande wa minada wa Saragana zimetolewa sh. 7,00,000/= kwa ajili ya ujenzi wa choo na mwamba wa kuchinjioa mifugo. Pamoja na kutolewa kiasi hicho cha fedha kikao kiliendelea kusisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wananchi kuchimba mashimo ya choo na Halmashauri itoe vifaa vya kujenga ili kupunguza gharama

   Baada ya maelezo hayo

   Kamati iliazimia

   Kuwa, suala la usafishaji wa stendi mpya na minada taarifa yake iwe inaletwa mara kwa mara kila kamati ya fedha inapokutana ili kujua hali ya utekelezaji wake.

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/116 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA MWEZI MEI,2017.

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa, pamoja na taarifa hiyo pia iligundulika kwamba vipo vyanzo vya mapato ambayo kwa mwezi April havikukusanya na pia vipo vyanzo vya mapato ambavyo havikuonyeshwa kwenye taaarifa ya mwezi mei vyonzo hivyo ni pamoja maegesho katika mwalo wa Kasoma, Esira, Kiemba n.k

Aidha katika kudhibiti mapato kikao kilikubaliana kuweka kizuizi katika barabara Nyegina mkrira ambako kunapitishwa samaki wengi kuletwa mjini bila kutoa ushuru. Pia mkurugenzi Mtendaji (W) alitakiwa aende kuona/kujifunza jinsi Halmashauri ya Wilaya ya Butiama inavyokusanya mapato yake kutoka kwa wachenjuaji wa dhahabu ili Halmashauri iweze kukusanya mapato hayo. Mwisho wajumbe walimtaka mkurugenzi mtendaji (W) na Mweka hazina kuona uwezekano wa kulipa madeni ya Waheshimiwa Madiwani.

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/117 TAARIFA YA MABADILIKO YA WAWEKA SAINI BENKI KWA WAKUU WA IDARA WANAOKAIMU

Akiwasilisha taarifa hiyo Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema, kutokana na idara za fedha na Mipango kuwa na Mkuu wa idara wanakaimu baada ya wakuu wa idara husika kuondolewa katika majukumu yao wafuatao walipendekezwa kuwa waweka saini.

1. Jesse mwangwa – Badala ya ndugu Kalwa Almas Mombo
2. Ndugu Jordan S. Ojode – badala ya Ndugu Mkama D. Lugina

Wajumbe kwa kauli moja walipitisha mapendekezo hayo.

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/118 MGAWANYO WA MALI NA MADENI

Ilisomwa barua iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kwa wakati huo kwenda kwa Katibu Tawala Mkoa juu ya mgawanyo wa mali na madeni kati ya halmashauri ya Wilaya ya Musoma na Butiama. Aidha wajumbe pia walipata ufafanuzi wa kina juu ya

mgawanyo huo kutoka kwa mjumbe aliyekuwa mwanakamati kwa wakati huo Ndugu Gerald mfungo Kasonyi. Akitoa ufafanuzi ndugu Kasonyi alisema mgawanyo ilionekana kwamba halmashauri ya Wuilaya ya Musoma inaondoka kwenda Suguti katika eneo la Kwikonero na Halmashauri ya Wilaya ya Butiama iende butiama. Hata hivyo alisema barua/waraka kutoka Serikalini wa kutaka halmashauri ya Wilaya ya Musoma kuhamia haupo bali Halmashauri ilitakiwa kuhama ni halmashuri mpya ya Butiama na Halmashauri mama ya Musoma kuendelea kubaki na kuendelea kutumia majengo yaliyopo.

Baada ya maelezo hayo

Kikao kilikubaliana yafuatayo:-

(i) Halmashauri ianze mchakato wa kudai mali za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma zisizohamishika kwa katibu Tawala Mkoa

(ii) Kwa kuwa mgawanyo huo haujatangazwa kwenye gazeti za Serikali kikao kilikubaliana kutengua maamuzi ya awali ya kuhamishia makao makuu murangi.

3. UMILIKISHWAJI WA VIWANJA VYA HALMASHAURI VISIVYO NA MGOGORO.

Akitoa ufafanuzi Mkurugenzi Mtendaji (W)alisema,suala hili linaendelea kufatiliwa kwa Katibu Tawala Mkoa,kikao kiliendelea kusisitiza jitihada zifanyike eneo la Halmashuri lipate hati ili tuweze kukopesheka.

3.WATENDAJI WANAOLALAMIKIWA

Kikao kilimtaka Mkurugenzi Mtendaji (W) awahamishe Watendaji wa kijiji cha Bwai na Rukuba pamoja na kuwachukulia hatua kwa kusababisha kukwamisha ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo hayo

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/52 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA DESEMBA, 2016.

Taarifa ya mapato na matumizi iliwasilishwa na kupokelewa, pamoja na taarifa hiyo wajumbe walisisitiza yafuatayo:-

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/119 MWEKEZAJI WA SHAMBA LA BUGWEMA.

Akitoa ufafanuzi Afisa Kilimo alisema yupo mtu kutoka Arusha anayetaka kuwekeza katika shamba la Bugwema, shamba hilo lina jumla ya hekali 5,000 lakini kwa kuanzia anaomba kukodishiwa hekali 3,000.

Timu ya Menejimenti imemtaka aje kuongea na Menejimenti, kwa mapendekezo ya timu ya menejimenti inamtaka mkodishaji huyo kulipia kwa kila heka sh. 50,000/= badala y ash. 10,000/= alizoainisha kwenye barua yake na mkaataba uwe wa miaka mitatu mitatu badala ya miaka 10. Na taratibu za mazungumzo bado zinaendelea pindi yakikamilika taarifa kamili itawasilishwa kwenye kikao hiki, kikao kilibariki utaratibu wa mazungumzo uendelee.

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/120 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa, hakuna hoja iliyojitokeza kikao kilipitisha taarifa hiyo.

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/121 TAARIFA YA GHARAMA ZA MAKISIO YA VIKAO VYA MABARAZA KUTOFANYIKA MURANGI.

Makisio ya gharama za uendeshaji vikao vya mabaraza ya madiwani kufanyika murangi yaliwasilishwa na kupokelewa, baadhi ya wajum,be hawakuafiki kupeleka vikao vya Mabaraza ya madiwani murangi na kwamba suala hili lipelekwe kwenye kikao hca baraza la madiwani kwa uamuzi zaidi

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/122 MENGINEYO

Hayakuwepo

KUMB.NA. KFUM/03/2016/2017/123 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 10.00 kamili jioni na kuwashukuru wajumbe kwa majadiliano alisisitiza ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuwapa mafuta makandarasi walikubali kusafisha maeneo ya stendji mpya

pamoja na barabara ya kwenda mwalo wa Nyamlinsa. Mwisho aliwatakia wajumbe wote mapumziko mema.

UMETHIBITISHWA

M/KITI ..... KATIBU .....

TAREHE 04-08-2017 TAREHE 04/08/2017